# *MATENDO YA ROHO MTAKATIFU*

. . .kuzunguka kanisa. Tulikuwa na ibada ya mazishi, alasiri ya leo, tuna nyingine asubuhi. Kwa hiyo nikasema, "Hebu twende kanisani, upesi sana sasa, ili tusikose yoyote ya hizo ibada."

2 Na sikujua ya kwamba Ndugu Neville angesema, "Njoo huku na ukaongee kidogo." Lakini nina furaha sana kupata nafasi ya kuwasalimu tena katika Jina la Bwana Yesu, kwa upendo na fadhili Zake, na rehema, kwetu sisi sote; na kwa ndugu yetu hapa, mchungaji.

3 Mnajua, Ndugu Neville ni tofauti kidogo na wahudumu wengi. Wananinii tu. . .wakati mhudumu, anapotoa mimbara yake, hilo ni jambo kubwa kwake. Hamtambui tu kuwa ni nini. Lakini, Ndugu Neville daima amekuwa mwenye upendo na mwenye kujali kila mara kutoa mimbara yake ninapoingia. Na kusema, "Ndugu Bill. . . " Na sio tu kukuuliza ikiwa unataka; kidogo anakushawishi uje, unajua. Na inakufanya ujisikie kukaribishwa maradufu. Nami ninafurahia sana jambo hilo, mnaona. Huwezi tu kukatalia mtu yeyote, namna hiyo. Wao ni wema sana na wazuri, kwa njia hiyo.

4 Nilimsikia akisema mtoto wake mdogo alikuwa akitapika na kuumwa. Nami. . .Ndugu Junior, naamini ilikuwa ni mtoto wake mchanga niliyemsikia akikohoa huko nyuma, dakika chache zilizopita. Je, huyo ni mtoto wako, Junior, ambaye alikuwa anakohoa? Na mafua mengi na kadhalika yakiendelea. Tutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa, baada ya muda mfupi tu.

5 Sasa, nitaanzia tu pale nilipoachia asubuhi ya leo basi, kwenye mlango wa 4 wa Matendo. Na kwa hiyo. . .Na kuanzia, naamini, kwenye yapata kifungu cha 10 cha mlango wa 4 wa—wa Matendo ya mitume, au, matendo ya Roho Mtakatifu katika mitume. Mnaona? Daima tunafikiria hivyo, tunaita hicho, "Matendo ya mitume." Lakini hayakuwa ni matendo ya mitume. Ilikuwa ni Roho Mtakatifu ndani ya mitume, akitenda, mnaona. Hao wanadamu, wenyewe, walikuwa ni wanadamu, wala hawakuweza kutenda. Kabla sijaenda mbali zaidi. . .

6 Nilikuwa nimeketi nyuma pamoja na Ndugu Wood, dakika chache tu zilizopita. Na jamaa fulani mdogo, ambaye amekuwa hapa kanisani kwa muda mrefu, daima ametaka kupata mahali pake. Ninaamini ningeweza kumwambia, kama tu angefanya hivyo. Ni kuimba. Ndugu Temple, u—unaweza kufanya jambo moja na jingine, lakini wewe ni mwimbaji mzuri. Kwa hiyo na—nathamini hilo. Na kama ukijiachilia tu, kwa uimbaji, Mungu angekutumia. Lakini u—unaninii. . .?. . .uko kwenye kila kitu

kingine ila jambo sahihi. Ingia katika uimbaji. Hicho hapo kipaji chako. Huna budi kukitumia hicho. Ajabu. Ninapenda uimbaji huo wa kale, nanyi je? Naam, bwana. Kusikia huo, huko nyuma namna hiyo, naupenda huo, Ndugu Neville. Hakika naupenda. Mmoja . . .

7 Ninafurahia mahubiri ya Ndugu Neville na kila kitu. Nami bila shaka nafurahia uimbaji huo mzuri wa kale ambao yeye na hao dada huimba, pia, kwenye kipindi cha re—redio. Ikiwa nyote hamjawahi kuzisikia bado, wengi wenu, mbona, ifungulieni kila Jumamosi asubuhi mwasikilize, na hakika mtabarikiwa. Mbona, mke wangu na watoto wangu, na kila mtu, anatazamia kipindi hicho, kama tu vile ingalikuwa ninaenda kuwa huko chini mimi mwenyewe, nami nilikuwa kule chini, mmoja wa wa—wapendwa katika familia. Tunatazamia mimbara hiyo, ama kipindi hicho, Jumamosi asubuhi, nasi tunakifurahia sana.

8 Mnajua, asubuhi ya leo kulikuwa na jambo fulani lililotukia hapa ambalo si—siwezi kulisahau bado, lilikuwa lile lililomhusu mtoto yule mchanga. Nilikuwa na hisia ya ajabu sana kuhusu hilo. Nami nashangaa tu. Nilipoamka asubuhi ya leo, nilimtazama mke wangu na kusema, "Mpenzi, a—ama nilikuwa na ndoto au ono. Nami," nikasema, "Si—sitasema lilikuwa ni ono, kwa sababu huenda nilikuwa nimelala. Lakini," nikasema, "ni halisi tu sana! Nami nilikuwa nimeketi mle chumbani wakati lilipoisha." Nikasema, "Sikumbuki, hata hivyo, nilipoamka kuninii . . . kwenye hilo ono, liliponigusa."

9 Lakini nilipofika hapa chini, ilininii . . . na kuona mambo hayo yote yakiendelea mbele vile tu. Nami nilikuwa nimempigia simu Dada Cox na kumwambia, siku chache zilizopita, kuhusu mtoto mchanga wa aina hiyo hiyo. Na hapana shaka huyo alikuwa ndiye yule mtoto. Na jamaa huyo mdogo, macho yake yameliwa na kansa. Jicho lake dogo, hapa, limetoweka, na ni ganda tu linalotokeza mle. Imeingia kwenye jicho lingine, naye huyo mtoto amelala tu bila uhai. Na daktari mmoja maarufu wa upasuaji Louisville, alimwambia mama huyo amlete hapa kwangu, aombewe. Basi hiyo ndiyo . . . Na hivyo wote . . . Ninaamini tu kwamba Mungu alikuwa akileta . . . alikuwa ametoa ono kwa ajili ya mtoto huyo. Na hakika tu kama ninavyoamini nimesimama kwenye jukwaa hili, usiku wa leo, mtoto huyo ameponywa. Naam, bwana. Mimi tu . . . Mimi mara chache sana, Ndugu Cox, huwa nachanganyikiwa katika mambo ya aina hiyo.

10 Sasa, nilichanganyikiwa wakati mmoja, sikuweza kueleza wazi juu ya Ndugu George Wright, wakati ningeninii . . . Ndugu McDowell alikuwa ameniita, ili—ili kwenda kazini kwake, au kwa mamake Charlie kule juu. Naye alikuwa amelala hospitalini bila uhai, karibu. Naye Ndugu Mack alitaka niende, kwa hiyo ni—nikapanda kwenda kumwona huyo mtoto. Nami nilikuwa nimeshuka kwa Ndugu George siku nne. Nami nilimpenda.

Lakini kwa moyo wangu wote naamini alikuwa anatuacha. Hiyo ni kweli. Ninaamini alikuwa yuafa. Nao madaktari, "Hakuna nafasi kwake." Vidonge vya damu vikienda moyoni mwake, kwa hivyo hakukuwa na kitu chochote kingeweza kufanywa.

11 Bibi Wright, aliyeketi hapa, dada yetu, aliuliza niliyowazia juu yake. Baada ya siku nne za kumwombea, nilisema, "Naamini amekwisha."

12 Naye mtoto Edith akaniuliza kuhusu hilo. Nisingemwambia. Nilisema, "Loo. . . " Lakini bado alikuwa na imani. Aliamini. Alishikilia. Nami. . .

13 Ndugu Shelby ameketi kule nyuma, kama tu kwamba alikuwa ndugu yangu wa kuzaliwa. Alikutana nami huko nje, akasema, "Unafikiria nini kuhusu baba?"

14 Nikasema, "Shelby, ninaamini anatuacha." Nikasema, "Ninaamini a—anatuacha." Nikasema, "Vema, ana umri wa miaka sabini na mitatu, naye amemaliza wakati wake wa maisha. Naye Mungu alimwahidi tu sabini." Nikasema, "Naamini amekwisha."

15 Na usiku huo niliporudi nyumbani kutoka kule chini, Ndugu Mack alishikilia tu kwamba niende kule. Naye Charlie akanipeleka huko, mbali. . . Akafika huko juu, wala hakurudi tena mpaka usiku sana, ama mapema asubuhi. Nami nikaenda tu na kumwombea huyo mwanamke, ndilo tu ningaliweza kufanya.

16 Ndipo niliporudi nyumbani, nikaingia chumbani, nikavua nguo na kujitayarisha kulala. Basi nilipofanya hivyo, nikasikia mtu akizungumza. Nikaangalia huko, na kulikuwa na mwanamke mwenye mvi. Naye alikuwa amesimama jikoni, akizungumza na mtu fulani kwenye simu. Ndipo ikatokea kuwa, ilikuwa ni mama wa mvulana huyo. Hiyo ni kweli. Nami. . .

17 Ndipo nikauona ma—maskini ule mkuyu karibu papo hapo kando ya nyumba ya Ndugu George, nami nikaona mabonge yakianguka, ya matope au uchafu, yakionekana kama udongo. Na yalikuwa ni uchafu, na yalikuwa ni matope. Naye akasema yalikuwa ni "kaburi." Kitu kuhusu kaburi, "Na kuhusu wengi wa wale waliokuwa wakimcheka, wangemtangulia kaburini," ama kitu kama hicho. Nami nisingeweza kulielewa vizuri. Kwa hiyo, upesi, nikamshika Dada Wright, na kumpigia simu na kumwambia (Dada Wright, naamini alikuwa ndiye) kwamba sikuelewa hilo ono jinsi lilivyokuwa.

18 Hata hivyo, mama yake Charlie akaenda nyumbani, na alikuwa nyumbani na kuzungumza kwenye simu, na kila kitu kama tu lile ono lilivyosema. Nafikiri ameaga sasa. Lakini, alienda nyumbani kama tu lilivyosema, wakati waliposema hata hangeweza kuishi hadi asubuhi; lakini aliishi. Sasa, na hilo lilikuwa tu ni kuhusu Mungu kutujalia kujua kwamba alikuwa amejibu maombi yetu.

19 Mtu fulani aliuliza, hivi majuzi, au ama hu—huyo mtu aliandika kitabu hivi majuzi, kasema, “Mwanaume aliyekuwa na tatizo la tezi dume, na,” kasema, “aliponywa. Na mwaka mmoja baadaye, akasema alikuwa mgonjwa tena.”

20 Mbona, kabisa. Unaweza kuponywa usiku wa leo, na kuugua tena asubuhi, kwa kitu kile kile. Unaweza kuwa mwenye dhambi usiku wa leo, na ninii . . . Unaweza kuwa mwenye dhambi usiku wa leo, na Mkristo asubuhi. Unaweza kuwa Mkristo usiku wa leo, na mwenye dhambi asubuhi. Hakika.

21 Daktari anaweza kumpa mtu penisilini kwa ajili ya homa mbaya au nimonia, na kumponya sasa hivi. Na wangeweza kufanya uchunguzi; awe mzima kabisa, hamna nimonia juu yake, au homa; na kesho yake anaweza kufa kwa nimonia, kitu kile kile. Je, hiyo ni kweli? Hiyo haina uhusiano wowote nao.

22 Mnaona, ni, “Kumchuja mbu, na kumeza ngamia,” hilo kama msemo wa kale ulivyo.

23 Lakini, hata hivyo, basi, nikirudi na kumwambia Dada Wright. Nikaenda basi, nami nikaona ono tena, na kumwona Ndugu George Wright ameketi pale nyuma, nami nikiingia mlangoni. Alishuka moja kwa moja kupitia kwenye marefu haya ya kanisa, kisha akaenda moja kwa moja pale na kunipa mkono, akitembea.

24 Asingeweza kutembea; nyote mnajua hali yake. Bonge la damu lilikuwa limeipindua miguu yake chini namna hiyo, naye daktari akasema, “Linaingia moyoni mwake. Angekufa wakati wowote.” Kwa hiyo, akiwa na umri wa miaka sabini na mitatu, hapakuwepo na nafasi hata kidogo ya kuishi.

25 Nami nikarudi na kuliambia kanisa, nikampigia simu Dada Wright. Isitoshe, bali nilishuka huko. Na huko nyumbani kwake, watu . . . Watu wawili walikuwa wameketi nyumbani mwake, naamini, asubuhi hiyo. Sivyo, Ndugu George? Watu wawili walikuwa nyumbani mwako, asubuhi nilipokuja kule. Yule jamaa jirani na jamaa mwingine mkubwa. Nikasema, “Loo, naam . . . ” [Ndugu George Wright anasema, “Hapana shaka ulizungumza nao. Sikumbuki.”—Mh.] Ati nini bwana? [“Hapana shaka ulizungumza nao. Sikumbuki.”] Naamini . . . Sivyo, Edith? Naam, na kulikuwa na wawili. Naam, alikuwa katika hali mbaya.

26 Lakini nikasema, “Usiruhusu jambo lolote likusumbue, kwa sababu Ndugu Wright anakuja maskanini, akitembea tena, kwa kuwa ni BWANA ASEMA HIVI.”

27 Nilichanganyikiwa juu yake. Nikasema, “Kuna kitu kuhusu kaburi.” Na kile kilichokuwa wakati huo, wakati nilipofunuliwa hilo ono wazi, jambo ni kwamba, ilikuwa ni wale waliomdhihaki kuhusu kuacha kanisa alilokuwa nalo, ambao hawakuamini

katika uponyaji wa Kiungu. Naye angeona makaburi yao yakichimbwa, na kujua kwamba wangemtangulia kuondoka.

28 Ni wangapi wamesalia, tangu wakati huo? [Ndugu George Wright anasema, "Wanne au watano wamekwisha kuzikwa tangu nipate nafuu. Naye mhubiri wangu aliyenihubiria nikaliacha kanisa langu, alifukuzwa yapata majuma mawili yaliyopita."—Mh.] Je, Bwana ni mkweli? Naam, bwana. Ndivyo nilivyo hakika. Hao ni watano kati ya...Hao ni wanne, na huyo, hao watakuwa watano. Watano wameaga. Wala haijapata mwaka bado, sivyo, Ndugu George? ["Karibu tu mwaka mmoja."] Takriban mwaka mmoja, wakati huu. Hivyo ndivyo ilivyokuwa, mnaona. Bwana anapozungumza, ni kamilifu kabisa. Unaweza kulifuatilia moja kwa moja. Sijawahi kuona hata moja likishindwa. Na haijalishi ni nini, ikiwa...

29 Madaktari wetu wapendwa na kadhalika wamemshughulikia mtoto huyo, na kila kitu kimefanywa. Sina hakika, lakini karibu nina hakika ya kwamba hilo ni jambo lile lile, kwa sababu nilimwona mwanamke huyo akiwa na vile vitu juu yake, mwajua, vipodozi midomoni mwake; na—na alikuwa amesimama mahali ambapo mazishi ya mke wangu yalihubiriwa. Na huyo mtoto alionekana kama mtoto wangu mchanga, Sara, kule nyuma, mnaona. Na huyo ndiye yule mtoto, karibu nina hakika. Ikiwa ndiye, hakuna kitu kingine chochote duniani...Lakini nilimwona mtoto huyo mchanga, kutoka mautini, akifufuka. Mnaona? Naye ataishi, kwa hakika kama vile Mungu alivyo Mbinguni usiku wa leo, na Maneno Yake ni ya kweli. Naam, bwana. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Kwa hivyo, tutaangalia na kuona. Bwana ni wa ajabu. Sivyo? Jinsi alivyo mwema kwetu!

30 Sasa tulikuwa tukijifunza, asubuhi ya leo, katika Kitabu cha Matendo, kuhusu Kanisa, likiwaka tu kwa utukufu wa Mungu. Jinsi Bwana Yesu alivyokuwa amekuja tu kama shahidi, duniani, ya kwamba Yeye alikuwa Mwana wa Mungu! Jinsi walivyokuwa na imani kuu Kwake! Na jinsi alivyokuwa amewaambia kwamba haikuwezekana Kwake, katika mwili wa nyama, kuwa ndani ya kila mtu! Angeweza tu kuwa katika mwili mmoja. Lakini basi, kama angeenda Zake, angerudi tena katika umbo la Roho, halafu basi angekuja kwa kila moyo wenye njaa ambao ulikuwa na njaa na kiu kwa ajili Yake. Na kazi zile zile alizofanya hapa duniani, Yeye angeziendeleza katika Kanisa Lake, hata ukamilifu wa dahari.

31 Hivi hamna furaha kwamba mko katika Kanisa hilo, usiku wa leo? Sio chini ya...Sio hili, hili—hili paa la kanisa. Ninamaanisha, katika Kanisa. Kuna Kanisa moja tu. Wa—wala hujiungi nalo. Hu—huwezi kupeleka karatasi, ndani Yake. U—u—unazaliwa tu ndani Yake, hivyo tu. Nawe umezaliwa katika Kanisa hilo, na ni kwa neema kwamba umezaliwa ndani Yake. Hungeweza kuona njaa kuingia ndani Yake; huna

hamu Nalo, unachukia wazo Lake lenyewe, isipokuwa Mungu mwenyewe amekusudia kwamba uwe katika Kanisa hilo. Na kama ulikuwa. . . Ikiwa utawahi kuwa katika Kanisa hilo, Mungu alijua hilo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ya kwamba ungekuwa katika Kanisa hilo. Naye alilikusudia, na kukuchagua tangu zamani uwe katika Kanisa hilo. Si ajabu hiyo?

32 "Wote wanaoisikia Sauti Yangu watakuja Kwangu." Je, hiyo ni kweli? "Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu, nami nitamfufua tena siku ya mwisho."

33 Angalieni, sasa, watu wanasema, "Siamini katika mambo kama haya!" Usiwadharau. Waonee huruma, unaona. Waombee. Kwa sababu ha—hawana kitu *humu*, na pengine hawatapata kitu, cha kuaminia. Wanaamini kutokana na m—mtazamo wa kitheolojia. Wanasema, "Vema, naam, ninaamini ya kwamba hiyo ni ninii tu. . . " Lakini, ninamaanisha, hawawezi kuamini isipokuwa ni Mungu kweli aliye moyoni. Mnaona? Wala huwezi. . .

34 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Sio kwa sababu alijiunga na kanisa, sio kwa sababu alibatizwa, sio kwa sababu alifanya *hivi*, kwa sababu alipaza sauti, kwa sababu alifanya hili *lingine*. Mambo hayo ni sawa; kujiunga na kanisa, kubatiza, kupaza sauti. Lakini Yeye alisema, "Yeye aliye na Uzima wa milele, kwa sababu ameamini."

35 Sasa, katika Matendo 2:38, Petro alisema, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

36 Nami nimeshangaa, kwa miaka mingi, wakati ningeona hilo na kulisoma. Niliwazia, "Bwana, hawa hapa wanaume na wanawake wanakuja. Nimewaona wakija madhabahuni, na kupiga magoti na kulia, na kuomba, kwenda na kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu, na katika juma moja baadaye, wako huko nje pamoja na ulimwengu tena." Nikawazia, "Ee Mungu, hakika Neno Lako halina makosa. Kamwe siwezi kulielewa. Lakini Wewe, Bwana, kama nitaendelea pamoja Nawe, ulisema Neno Lako litakaa ndani yangu."

37 Kwa hiyo niliendelea Naye, mpaka sasa ninaona ni nini. Amelifanya lijulikane, mnaona. Nami sikulijua kamwe mpaka Bwana alipolifungua tu, siku moja, na hilo hapo limewekwa mbele yangu. Ndipo nikaona watu hao hawakuwa vile walivyokuwa hapo mwanzo, mnaona, kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Sio yeye anayetaka kuwa; ni Mungu anayelichagua liwe. Si kama unalitaka, ama hulitaki; huna uhusiano wowote nalo. Ni Mungu. Yeye, "Humfanya mgumu yeye amfanyaye mgumu. Humrehemu yeye atakayemrehemu." Hiyo ni kweli. Na haijalishi wewe ni

nani, una wadhifa gani, kama wewe ni rais au kama wewe ni ombaomba mtaani, haileti tofauti hata kidogo. "Mungu humrehemu amrehemuye."

38 Na kabla ulimwengu haujaanza, Yeye alichagua kwamba kiasi fulani cha watu, kote katika nyakati, kwamba walikuwa ni akina nani, wangeokolewa. Na kila aliyemchagua atamjia. Hiyo ni kweli. Kila mmoja atakuja, wala hakuna hata mmoja wao atakayepotea. Amechagua, kasema kutakuwa na Kanisa kule; litakuwa bila waa; litakuwa bila kunyanzi.

39 Na sasa, nyakati zilipozidi kusonga, nasi tuliziona asubuhi ya leo, katika somo, na hao walimu wakuu wa Kiorthodoksi, mashuhuri tu na walioadibishwa wawezavyo kuwa, watakatifu tu wawezavyo kutembea duniani. Nayo Biblia...Sikilizeni. Biblia ilisema, "Walionekana hawana lawama." Maana, walisema, "Loo, nisingegusa *hilo*. Nisingefanya *hivi*." Mnaona, lakini hiyo haikuwa ni neema; hiyo ilikuwa matendo.

40 Nasi hatuokolewi kwa matendo, yale tunayofanya. Sio kile nilichofanya ambacho kiliniokoa. Ni kile Kristo alifanya ndicho kilichoniokoa. Mnaona? Si kile...Sina utakatifu wowote.

41 Ikiwa ningejaribu kusema, "Vema, niliacha kunywa pombe. Niliacha kuvuta sigara. Niliacha kuiba, kusema uwongo, na kadhalika." Hilo ndilo nililofanya, mnaona. Hilo lingekuwa ni langu mwenyewe. Ningekuwa na kitu cha kujivunia.

42 Lakini si—sikuacha chochote. Alinijia tu na kuniondolea. Unaona? Ndivyo ilivyo. Basi si kile nilichofanya. Ni yale aliyofanya.

43 Na, basi, Roho Mtakatifu basi hukaa ndani, na kukua kila siku; hukua tu, akijifanya Mwenyewe kuwa mkuu zaidi na zaidi; husukuma mambo nje, mahangaiko, majaribu. Unapoyashinda, Roho Mtakatifu anachukua mahali Pake. Unajua nini? Ikiwa una jaribu baya sana la kitu ambacho si sawa; shinda kitu hicho mara chache, na uangalie kama ushuhuda wako haupanuki kwa sababu yake.

44 Mwangalie Samsoni. Alipopata...Simba akakimbia apate kumwua, naye akamwua huyo simba wakati Nguvu za Mungu zilipomjia. Akamwua kwa mkono wake mtupu, labda tu akapasua taya zake. Maskini, mdogo sana, mwenye nywele za mawimbi, yapata urefu *huo*. Maskini jamaa mdogo, aliyekonda, mtaani; vishungi saba vidogo vikining'inia kichwani mwake, kama maskini dondoadume. Naye hakuwa zaidi ya maskini dondoadume mdogo, mpaka Roho wa Mungu alipomjia.

45 Sasa, haingekuwa vigumu kuamini kwamba jitu kubwa mno lingeweza kumwua simba kwa mikono yake. Naamini angeweza kufanya hivyo. Lakini jambo la kuchekesha lilikuwa, maskini jamaa huyu mdogo sana alifanya hivyo.

46 Lakini Roho wa Bwana akamjia, naye akamwua huyo simba, akamtupa upande mmoja. Nao nyuki wakajenga mzinga wao mle ndani. Naye Samsoni . . . asali tamu zaidi aliyowahi kula, ikatoka kwenye ule mzinga wa yule simba aliyeuawa. Hiyo ni kweli? Kwa nini? Alimshinda kwa Nguvu za Mungu.

47 Na kama una kitu unachotaka kula asali tamu kutoka kwake, kishinde tu kwa Nguvu za Mungu. Hiyo ni kweli. Tazama jinsi lilivyo zuri. Loo, jamani. Pitia . . . Labda umekuwa mlevi, na, hata hivyo, kila wakati unaponusia wiski ama pombe, ama chochote kile, unataka kuinywa. Ishinde, kwa Nguvu za Mungu; na upitie hapa wakati mmoja, uone ni hisia ya namna gani uliyo nayo moyoni mwako, wakati kitu hicho kimekwisha kufa na kutoweka basi, chote kimekwisha. Loo, jamani, asali hiyo tamu unayopata kutoka kwake!

48 Sasa, watu hawa walikuwa wameshinda kweli. Kwenye Siku ya Pentekoste, wote walijazwa na Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu zilikuwa juu yao. Walikuwa na karama walizopewa, kunena kwa lugha, na kila kitu. Walikuwa tu na wakati wa ajabu, na Kanisa lilikuwa linawaka moto.

49 Sasa nitaliendea kutoka kwa mtazamo mwingine mdogo hapa, kutoka kwa Stefano, kwenye wakati huu, hata nitakaporejea kwenye somo langu la asili tena, nikiweza. Angalieni, kuna mtu anayeitwa Stefano. Hakuwa mmoja wa wale mitume. La, hakuwa. Alikuwa tu shemasi. Lakini, loo, ndugu, akapata kitu fulani moyoni mwake. Asingeweza kusimama kimya.

50 Hivyo ndivyo kila mtu alivyo anapoliweka moyoni mwake. Kamwe huwezi kustahimili; jamani, hana budi kumwambia mtu fulani!

51 Nao hawa hapa, huko nje mtaani, wakifanya uamsho, na wakiwa tu na wakati mzuri sana. Mbona, ilikuwa kama nyumba inayoteketea, katika upepo mkali. Kamwe usingeweza kumkomesha. Hivyo tu.

52 Kwa hiyo wakamchukua, chini barabarani, na kumkokota kwenye Baraza la Wazee. Kasema, "Ndugu, tutamrekebisha jamaa huyo. Tutakomesha ulokole huu wote." Nao wakamtia gerezani mpaka asubuhi. Baraza la Wazee likakutana, labda watu nusu milioni, au zaidi, wamekusanyika huko nje. Wakamsukumia maskini Stefano huko nje.

53 Lakini alipotoka, ndugu, alitoka, nao uso wake ukang'aa kama Malaika. Ndugu, siwazii, kama nuru inayomulika, bali uling'aa kwa uso, ambao ulijua alichokuwa akizungumzia. Sidhani kama Malaika angekuwa kama mwanga, mwanga au kitu kinachong'aa. Lakini ilimaanisha aling'aa na hili, kwamba alielewa kile alichokuwa akizungumzia.

54 Biblia ilisema kwamba alikuwa na ujasiri. Akatoka huko nje, kwa ukali, na kusema, "Enyi watu wa Israeli..." Akisimama peke yake, kama mwana-kondoo kati ya mbwa-mwitu elfu kumi wenye njaa wanaosaga meno kwa ajili ya damu yake. Kasema, "Enyi watu wa Israeli, nanyi nyote mkaao Uyahudi, na kadhalika, na akina baba! Na ijulikane kwenu, Mungu wa Ibrahimu...Mungu wa baba zetu alimtokea Ibrahimu, akampandisha kutoka Ukaldayo, akampa ahadi ya nchi hii. Na—na kwa njia yake akaletwa Yesu Kristo, ambaye ninyi, kwa mikono mikatili, mmemsulubisha na kumwua."

55 Na alipomaliza kusema hayo, akasema, "Enyi, wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu! Kama baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo!" Loo, jamani! Ningependa kusikia mahubiri hayo kwenye rekodi. Ndugu Beeler, laiti tungelipata hiyo. Naam, bwana. Akasema, "Loo, enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu! Kama vile baba zenu walivyofanya, nanyi ni vivyo hivyo!" Ndugu, hiyo haikuwa ni kupunguza nguvu za mashambulizi (sivyo?), wakati akijua damu yake ingemwagika namna hiyo.

56 Biblia ilisema, "Alikuwa mtu aliyejaa..." Aliyejaa nini? Aliyejaa upumbavu? La, bwana. Aliyejaa theolojia? La, bwana. "Alikuwa amejaa Roho Mtakatifu." Hapo ndipo sifa hizi zote kuu, nzuri ziliwekwa, kwa sababu alikuwa amejazwa. Ulimwengu ulikuwa umesukumiwa nje, naye Roho Mtakatifu alikuwa ndani yake. "Alikuwa mtu aliyejaa Roho Mtakatifu." Jamani! Ati umzuie? Usingeweza kufanya hivyo. Hungeweza kumzuia. Alikuwa anawaka moto, ndugu. Ilimbidi kuihubiri Injili. Naye akaihubiri Injili, na kufanya miujiza na ishara.

57 Ndipo baada ya kitambo kidogo, walipomsagia meno, wakamkokota kutoka barazani na kumtoa pale, na kumwua. Nao wakamtupia madonge na mawe, hata wakamponda-ponda hata kufa. Huyo hapo Paulo amesimama, akishuhudia hilo, ndipo Paulo alipotazama chini na kumwona Stefano akifa. Stefano alitazama juu na kusema, "Naona mbingu zimefunguka. Ninaona mbingu zimefunguka na Yesu amesimama kwenye mkono wa kuume wa Mungu."

58 Paulo akatazama chini. Nawazia alikuna kichwa chake, akawazia, "Ni nini kinachoendelea?"

Akasema, "Bwana, usiwahesabie dhambi hii."

59 Kisha akalala usingizi mikononi mwa Mungu, akapembezwa. Kwa nini? Hakuhisi jiwe lingine tangu wakati huo na kuendelea. Mungu alimpembeza akalala mikononi Mwake, kama vile tu mama angemfanyia mtoto wake mchanga anayenyonya. Mungu alimchukua akampeleka vifuani mwa Kristo, kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu huko ng'ambo, ambako yuko katika amani; naye akahesabiwa miongoni mwa

wafia imani, akiwa na taji ya mfia imani kule usiku wa leo, "asiyepatikana na mauti," amesimama miongoni mwa watu. Huyo alikuwa ni Stefano, aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Madonge yalipoteza tu hisia zao, hayo mawe makubwa, yalipokuwa yakigonga kichwa chake. Mungu alimpembeza akalala usingizi. Biblia haikusema kamwe kwamba alikufa. Biblia ilisema, "Akalala." Amina. Hivyo ndivyo Wakristo wanavyokufa. Amina. Vema.

60 Sasa walikuwa na wakati mzuri sana. Ripoti hiyo ikarudi; kama vile Ndugu Neville alivyosema, muda mfupi uliopita. Sio tu. . . kidogo ikawapa hao mitume majivuno, na kadhalika. Ilibidi wafanye jambo fulani kulihusu. Moja kwa moja, hao wakaenda zao tena, upesi kama walivyoweza kwenda, wakihubiri Injili. Petro na Yohana, watu wawili wasio na elimu, wala maarifa, wakapita kwenye lango liitwalo Zuri. Jamani!

61 Ibilisi akasema, "Vema, sasa, wako huko tu wakihubiri, kwa hiyo haitadhuru chochote." Basi, watu hawa wote wanaamini katika kuhubiri, kila kitu.

62 Lakini walipopita katika lango liitwalo Zuri, pale alilala mtu mmoja. Roho Mtakatifu akasema, "Petro, mtu huyo anaweza kuponywa. Anayo imani." Alipoona kuwa alikuwa na imani ya kuponywa, alisema, "Simama kwa miguu yako." Naye akamnyanyua, akamshika mpaka mifupa yake ya kifundo cha mguu ikapata nguvu. Naye akaenda, akisimama na kurukaruka na kumsifu Mungu. Unajua nini? Hilo lilisababisha matatizo zaidi kuliko mahubiri yote waliyowahi kufanya.

63 Ndugu, acha tu jambo la upande wa ajabu lianze, ndipo uone jinsi kila mbwa laghai, kuzimuni, anavyoanza kumpigia makelele, akitamani damu sana. Hiyo ni kweli? Kweli.

64 Nawaambia, Petro alihubiri somo kwenye Siku ya Pentekoste, ndipo watu elfu tatu wakaokoka. Ibilisi hata hakuwahi kutoka kitandani mwake. Hiyo ni kweli. "Loo, vema, waacheni." Mnaona?

65 Lakini alipitia kwenye lango liitwalo Zuri, kesho yake, akamponya mtu, aliyelemaa tangu tumboni mwa mamaye, ndipo mambo yote yakamvurugikia. Hiyo ni kweli. Wakamtupa gerezani na kumweka humo usiku kucha. Naam, bwana. Mtieni gerezani, chumba cha ndani mle, kwa sababu ya hiyo ajabu. Ibilisi akasema, "Siwezi kuruhusu jambo hili lianze sasa, uponyaji wa Kiungu. Wakifanya hivyo, hakika watagonga mihimili yangu waiondoshe chini yangu." Hiyo ni kweli. "Maana, huenda nikawapumbaza, kote, kwa theolojia ndogo, mara moja moja. Lakini hakika siwezi kukipumbaza Kitu hicho halisi kinachotokea, na watu wamekiona kikifanywa. Nitalikomesha tu jambo hili kabla lile kundi lingine halijaingia ju—jukwaani."

66 Kamwe hakukizuia wakati huo. Hawezi kukizuia sasa. Hiyo ni kweli. Injili ya Mungu itaendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea. Na wakati hakuna mbingu tena ama dunia tena, Neno hilo litabaki lile lile. "Kwa maana mbingu na nchi zitapita, lakini Maneno Yangu hayatapita kamwe." Hayawezi kupita. Hayo Maneno hayawezi kufa kama Mungu Mwenyewe asivyoweza kufa. Haliwezi kufa. Ninaamini kila Neno Lake. Mambo yote ambayo Yesu alikuwa, ndivyo alivyo sasa, na daima atakuwa. Hiyo ni kweli. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

67 Roho Mtakatifu yeye yule aliyeshuka katika Siku ya Pentekoste ndiye Roho Mtakatifu yeye yule wa siku hizi. Nitakubali limekanyagiwa chini, likadhihakiwa, likafasiriwa vibaya, likawakilishwa vibaya, na kila kitu kingine kama hicho; huyo ni ibilisi tu, akiliigiza. Lakini kuna ubatizo halisi, wa kweli wa Roho Mtakatifu, unaoleta matokeo yale yale waliyokuwa nayo kwenye Siku ya Pentekoste. Hiyo ni kweli.

68 Hakika, Ibilisi ana chambo cha kale cha kunguru huko nje. Nawaambia Kweli. Kila wakati unapoona sanamu ya kuwafukuza ndege shambani, kumbuka, kuna kitu kizuri karibu. Hiyo ni kweli. Hakika. Huoni hiyo sanamu kwenye maskini mananasi…au namaanisha, tofaa za ua huku nje. Unaipata chini ya miti mikubwa mitamu, ambapo unaona hiyo sanamu ya kutishia, maana wanataka kuwafukuza. Ibilisi hubandika kila sanamu ya kutishia, dini nzuri sana ya Roho Mtakatifu, ambayo anaweza kuweka huko. Kwa sababu, mumo humo anakaa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliyefufuka, pamoja na Nguvu Zake zisizopatikana na mauti, yeye yule jana, leo, na hata milele. Amina! Hiyo inamaanisha "iwe hivyo." Vema.

69 Sasa, tunaona, waliwaweka katika gereza la ndani. Kesho yake asubuhi, wakawachapa kwelikweli, na kuwaachilia.

70 Sasa tunamwona Petro, asubuhi ya leo, akisimama miongoni mwao, hapa chini katika mlango wa 4. Naye akasema, "Mbona, enyi watu wa Israeli, na ninyi mnaokaa Uyahudi! Jambo hili na lijulikane kwenu. Yesu wa Nazareti, jinsi alivyothibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mtu wa Mungu. Ishara zote na maajabu ambayo Mungu alikuwa amefanya kupitia Yeye, yalithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mtu wa Mungu." Walijua ya kwamba Yeye alikuwa ni Mtu wa Mungu. Na kisha akasema, "Ninyi, kwa mikono miovu, mmemsulubisha na kumwua Mkuu wa Uzima; Ambaye Mungu amemfufua, na sisi ni mashahidi wake."

71 Kasema, "Kwa imani katika Jina Lake mtu huyu ameponywa." Kasema, "Ikiwa tukichunguzwa leo kwa ajili ya matendo mema tuliyoyafanya, na ijulikane kwenu, na nyumba yote ya Israeli, kwamba kwa Jina la Yesu Kristo mtu huyu ameponywa."

72 Walipouliza, "Ni—ni wa kundi gani la dini? Waliwekwa kama wahudumu chini ya lipi? Walitoka kwenye makaburi

gani?" Au kitu kingine kama hicho, "Haya yote yametoka wapi? Mlipata wapi haki zenu za kufanya hivi? Tuonyesheni kundi ambalo mnaliwakilisha, ili tuweze kurudi kwa wazee na kujua mnafanya hivi kwa sababu gani. Naam, bwana. Tunataka kujua ni fundisho gani la kanisa linalofundisha uzushi wa aina hii hapa. Mmetoka wapi?"

73 Petro akasema, "Katika Jina la Yesu Kristo, kwa njia ya imani katika Jina Lake, mtu huyu ameponywa." Amina.

74 Nao hawakuweza kusema lolote kuhusu jambo hilo, kwa maana hapo alisimama huyo mtu, nao walimjua. Amina. Amina.

75 Angalia, angalia alichosema hapa sasa.

> Na *hili ndilo lile jiwe* lililokataliwa na *ninyi waashi,* . . .
>
> *Wala hakuna wokovu katika* jina *lingine lo lote: kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo*.

76 Loo, kukataliwa kwa lile Jiwe! "Jiwe hilo lilikataliwa." Kwa nini? Walipojenga hekalu la Sulemani . . .

77 Nataka mwone picha nzuri sana hapa. Walipoanza kujenga hekalu la Sulemani, mawe yakachongwa, kutoka mahali pamoja, na mahali pengine, na mahali pengine. Baadhi yao yalikatwa *hivi*, na mengine *vile*. Lakini Biblia ilisema, ya kwamba, yalipoletwa pamoja . . . Ilichukua miaka arobaini, naamini, kulisimamisha lile hekalu. Wala hapakuwa na sauti ya msumeno, wala sauti ya nyundo, katika miaka arobaini. Yale mawe yakienda pamoja, jiwe juu ya jiwe; jambo pekee lililowabidi kufanya ni kupaka chokaa kidogo juu yake na kulilaza pale chini. Nayo yakashikamana, jiwe kwa jiwe, jiwe kwa jiwe. Wazieni hilo.

78 Sasa hili hapa wazo langu juu yake, ndugu. Wakati ninii . . . Hekalu lile pale liliwakilisha Hekalu, la kiroho, Hekalu ambalo tuko ndani yake sasa. Wanaingia hekaluni kwa ajili ya baraka zao. Tunabatizwa katika Hekalu la Mungu, katika Mwili wa Mungu, katika Mwili wa Yesu Kristo. Nasi tuko ndani ya Kristo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu; Wakorintho wa Kwanza 12. "Na sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu," Warumi 8:1, "wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho." Wanatamani mambo ya kiroho. Hawajali mambo ya kimwili.

Mwili wangu unasema, "Nimechoka mno."

79 Roho yangu inasema, "Hujachoka. Mimi ni Bosi wako. Nifuate." Amina.

80 Mnaona mgonjwa huko nje, naye daktari anasema, "Mnajua mgonjwa huyo hawezi kupona. Mgonjwa huyo amekwisha." Nitamwangalia, ninasema, "Hiyo ni kweli."

81 Lakini Roho Mtakatifu anakuja na kutoa ono, anasema, “Atapapata afya.” Kisha nasema, “BWANA ASEMA HIVI. Huyo mtu ataishi.”

82 Nasi hatufuati tena mambo ya mwili. Tunafuata mambo ya Roho. Hiyo ni kweli.

83 Sasa, wakati mawe haya yanapokuja pamoja. . . Yalikatwa, kote ulimwenguni, katika sehemu mbalimbali. Mbao na. . . zilizokokotwa kutoka kwenye mierezi yao mirefu ya Lebanoni, ikakatwa na kuletwa Yafa, kwa gari la ng’ombe, na kubebwa, na kadhalika, kwa chelezo cha magogo, mpaka yakaja kutengeneza he—hekalu. Lakini yanapounganishwa pamoja, hapana. . .

84 Nataka mtambue. Jiwe moja lilichongwa *hivi*, jiwe lingine likachongwa kwa njia nyingine. Labda, wakati waashi walipokuwa wakiyachonga, huenda walibishana na kugombana, na chochote kile.

85 Kama kundi la wahubiri linavyofanya siku hizi, “Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni church of God. Utukufu kwa Mungu, mimi ni wa Assemblies. Mimi *hili*.” Mnaendelea kugombana. Lakini, kumbukeni, Mungu Ndiye anayechonga.

86 Na wakati hili likikata *huku*, na moja *huko*, wasingeweza kuelewa. Lakini walipoenda kuyaweka pamoja, kitu hicho chote kilikuwa kimewekwa chini. Nao waliyaweka, bloku juu ya bloku juu ya bloku, wala haikuwabidi kuyachonga tena.

87 Ninaamini, moja ya siku hizi tukufu, wakati muungano huu wa umoja wa kanisa utakapoungana, kisha papa mpya atoke Marekani na kuwekwa huko juu kulingana na unabii, ndipo basi watafanya sanamu kama ya yule mnyama. Nami nawaambia, Kanisa la kweli la Mungu litaletwa pamoja. Waaminio halisi, wa kweli kutoka Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, Nazarayo, Pilgrim Holiness, wowote wale, wataungana, na kufungwa pamoja na upendo wa Mungu, hao wataufanya Mwili wa Bwana Yesu Kristo, waaminio wote. Nao wenye kushuku na wenye nia finyu watatupwa upande mmoja; wataingia moja kwa moja katika muungano wa makanisa.

88 Nami nilisoma hivi majuzi, hata Assemblies of God waliingia katika muungano wa makanisa. Loo, jamani! Inawabidi kukana mafundisho yao ya kiinjilisti, kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Na ishara zao zote na maajabu ya kipentekoste, kanuni, hawana budi kukana hayo, wapate kuwa katika muungano wa makanisa. Inawabidi kuyakana, loo, ndugu, wapate kuwa na hadhi.

89 Afadhali, kama nilivyosema mara nyingi, nilale njaa na kunywa maji ya tawi, na kula biskuti za magadi, na kupendwa na Mungu, na kuwa mtumishi Wake wa Mungu; kuliko kuwa na kilicho bora zaidi, ulimwengu huu utoacho, kama ilinibidi kupatana juu ya imani yangu katika Bwana Yesu Kristo na

Biblia Yake. Ninaamini *Hili* ndilo Neno la Mungu lisiloweza kukosea, na kila Neno Lake ni sahihi. Naam, bwana.

90 Sasa tutaangalia humo ndani jinsi walivyokuwa wakifanya. Walikataa . . . Walikuja, wakiyaweka mawe yao chini. Ndipo wakafika mahali, wakapata jiwe lililoonekana la ajabu-ajabu. Wasingeweza kutumia jiwe hilo. Wakasema, "Jiwe hilo halifai kitu." Nao wakalitupa, kwenye lundo la magugu mahali fulani. Wasingeweza kulitumia. Lilionekana ni la ajabu-ajabu. Nao wakajaribu kujenga jengo lao. Ndipo wakafikia mahali fulani, na kuweka mawe yote, na kuyalaza chini *hivi*. Wakafikia mahali, nao wasingeweza sasa kupata jiwe lolote la kuingia kwenye kona hii. Wakaendelea kujenga na kujenga na kujenga. Nalo hilo jengo likafika juu sana, lisingeweza kupanda zaidi, kwa maana walihitaji jiwe la pembeni. Wakatafuta kwenye mawe yote, wakijaribu kutafuta jiwe la pembeni, lakini hawakuweza kulipata. Na muda si muda mwajua, mtu fulani akaenda kwenye lundo la magugu. Nalo lile jiwe lenyewe walilolikataa lilikuwa ndilo jiwe kuu la pembeni.

91 Na ndivyo ilivyo siku hizi, enyi marafiki. Kanisa la Methodisti ni sawa. Kanisa la Kibaptisti ni sawa. Kanisa la Presbiteri, Pentekoste, Nazarayo, Pilgrim Holiness, lolote lile, yote ni sawa. Lakini jambo ni kwamba, ndugu, wanalikataa Jiwe halisi la Pembeni. Ndio maana Injili haijaenea ulimwenguni mwote, kwa nguvu na ishara na madhihirisho, ni kwa sababu madhehebu yamekata Nguvu zenyewe za mambo ya ajabu, yakisema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna kitu kama kunena kwa lugha. Hakuna kitu kama chochote cha kimbinguni. Hayo yalikuwa ni ya wakati uliopita."

92 Nawe utagundua, ndugu, ya kwamba, kila mmoja wao anayefanya hivyo, wamewekwa moja kwa moja kwenye rafu. Wao si zaidi ya mashirika ya vyama. Wana kundi la wenye kujiunga, hiyo ni kweli, lakini Biblia ilisema, "Wangekuwa na mfano wa utauwa, lakini wangekana Nguvu zake; hao nao mjieupushe nao."

93 Lakini kama makanisa, yanaona, madhehebu haya yote yamejaribu kujenga. Hawawezi kujenga juu ya kitu chochote pungufu ya Yesu Kristo na haki. Na kama ukimpokea Yesu Kristo, na kusema ni upumbavu . . .

Useme, "Loo, nilimpokea Yesu."

94 Ukimpokea Yesu, unapokea Kitu kinachokwambia, kwamba, "Neno hili la Mungu limevuviwa; Naye ni Bwana Yesu yeye yule, usiku wa leo, akitenda na kufanya mambo yale yale ambayo Yeye alisema angefanya," la sivyo hujampokea Bwana Yesu. Umepokea theolojia fulani, lakini si Bwana Yesu. Kwa maana Yesu anapoingia moyoni mwako, kuna jambo limetokea, hata unaamini kila kitu ambacho Mungu anasema.

95 Isitoshe, bali unajua ndivyo ilivyo. Mashetani wote kuzimuni hawangeweza kulitikisa kutoka kwako. Mbona, hakika, unaamini Hilo. Mungu tayari amesema hivyo, na hilo latosha. Wakati BWANA ASEMA HIVI, unaweka matumaini yako pale pale. Uishi au ufe, unaamini Hilo, kwa vyovyote vile. Uko tayari kutia muhuri ushuhuda wako kwa damu yako, wakati wowote, kwa maana unaamini ni Kweli. Unajua ni Kweli, kwa maana Mungu amesema hivyo. Na kitu Fulani ndani yako kinajua ni Kweli.

96 Lakini, sasa, kama ukiingia tu kutoka kwa mtazamo wa kielimu, na, mbona, unaweza kubishania *Hili* na kubishania *Lile*, na kusema, "*Hili* silo, na *Lile* silo. Nasi hatuamini *Hili*, na hatuamini *Lile*." Unajua, bishana. Unasema, "Loo, vema, siwezi kuamini kitu kama *Hicho*." Labda umefikia jambo lile lile New Albany, usiku wa leo; kubishana dhidi ya Mungu. Ni kwa nini?

97 Sikiliza kidogo zaidi, ujue maombi waliyoomba watu hawa:

98 Kasema, "Kwa nini mataifa wanafanya ghasia, na watu wanawazia ubatili? Kweli Bwana...ya Mwanao Yesu...na uwajalie watumishi wako," walipoomba kwa moyo mmoja, kasema, "wape watumishi wako, wanene—wanene Neno la Mungu kwa ujasiri, kwa kunyoosha mkono wa Mwanao, Yesu, kuwaponya wagonjwa..."

99 Amina. Mungu atusaidie tuwe na mkutano wa maombi namna hiyo! Nao walipokuwa wamekwisha kuomba, hilo jengo walimokuwa wamekusanyika lilitikisika. Loo, jamani. Hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo, wanaume na wanawake wenye moyo mmoja na nia moja, kama walivyokuwa. Hawazingatii *hili* ama *lile*, ama jambo lile lingine, bali umepotea katika Kristo Yesu. Matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu ya Damu ya Yesu na haki. Kama jua litachomoza kesho, au lisichomoze; tunajifunga pamoja kwa kiapo, mbele za Mungu, kwamba tutamtumikia Bwana Yesu na kutembea katika nyayo Zake, bila kujali gharama yake. Basi utakuta kanisa likiendelea. Amina. Kasema:

> *Wala hakuna wokovu katika* jina *lingine lo lote: maana hakuna jina—jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu, ambalo* mnapaswa *kuokolewa kwalo*.

100 Maskini mama mmoja anayehudhuria kanisa hili, yeye si mshirika wa hapa. Yeye ni Mmethodisti, lakini anatupenda. Naye huja kanisani.

101 Basi mama mwingine alisema, "Wewe huhudhuria kanisa gani?" Alimpigia simu. Nilisikia hili. Kasema, "Ni wapi, unahudhuria kanisa wapi?"

Kasema, "Ninaenda kwenye Maskani ya Branham."

102 Akasema, “Unamaanisha kwenda kule juu na kusikia Fundisho la namna hiyo, kuketi chini ya mambo kama hayo?”

Kasema, “Fundisho la aina gani?”

103 “Vema, wanajivunia Yesu kupita kiasi; kuhusu kubatiza, kutumia Jina Lake katika ubatizo, kutumia Jina Lake katika kila kitu kingine.”

104 Kwa maana Biblia ilisema, ndugu zangu, “Hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu, mpate kuokolewa kwalo.” Bila shaka.

105 Nakwambia, ndugu, mimi—mimi si mbishi. Lakini ningependa kumwona mtu yeyote, popote, wakati wowote, kwa Biblia, akithibitisha Hilo si sahihi. Hiyo ni kweli. Haijalishi wanasema nini, “Una wazimu,” na chochote kile; haileti tofauti yoyote.

106 Nikiwa nimesimama kwenye duka la vitabu, hivi majuzi, ambako nilikuwa naenda kununua vitabu. Ndipo mama mmoja akasema, “Nisingekuwa navyo kwenye rafu yangu. Siviuzi.” Kasema, “Mwanamke mmoja alikuja na kuvinunua vyote.” Alikuwa na saba, naye mwanamke huyu akavinunua vyote. Nadhani alitaka tu kuviondoa. Na kulikuwa na . . .

107 Mjadala ulitokea kuhusu uponyaji wa Kiungu. Hao hapo wahubiri wawili wa Kimethodisti wamesimama, na Mpresbiteri. Hao Wahubiri wa Kimethodisti, na mhubiri wa Kipresbiteri, walikuwa wakinitetea. Kasema, “Umesema kweli.” Nilipoanza kuondoka, nilishangaa nini . . . Ndugu Shire alikuwa amesimama pale, wakati uo huo. Ndugu Creech akaingia, wakati uo huo.

108 Wakati wote walipoanza kushuka chini, na kuanza kuzunguka-zunguka pale kidogo, mhubiri huyu wa Kimethodisti akajongea na kuweka mikono yake juu ya bega langu. Akasema, “Ndugu Branham, ulipokuwa si kitu ila mtoto, nilikuja mahali ulipokuwa umepanda juu ya nguzo, ukifanya kazi huku umevaa vichokoo, na uso mchafu.” Kisha kasema, “Nilijua ulifundisha uponyaji wa Kiungu. Na maskini mama yangu mkongwe alikuwa amelala mle ndani, akiwa na ugonjwa wa figo. Usingetibika. Alikuwa amelala, yuafa. Nawe ukaingia na kuvua vichokoo vyako, na kupiga magoti sakafuni na kumwombea mama yangu. Juma moja kutoka hapo, daktari alimtangaza kuwa ni mzima kabisa, amepona.” Kasema, “Hiyo imekuwa miaka ishirini na mitatu iliyopita, naye ni mzima kabisa na mwenye afya leo hii. Sijali kama ni kanisa langu, ama ni nini; ninaamini!” Haleluya! Hilo hapo.

109 “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Nyakati zinaweza kuja na kwenda, na mambo yanaweza kubadilika, lakini Injili ya Yesu Kristo itabaki kuwa ile ile katika nyakati zote zisizo na kikomo.

110 "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu." Kanisa hilo lilikuwa nini? Ulikuwa ni mwamba gani?

111 Hebu uliza kanisa Katoliki. Wanasema, "Ilikuwa ni jiwe kubwa lililowekwa pale. Kanisa Katoliki, ukasisi unaketi juu yake, usiku wa leo, 'juu ya mwamba huu,' kuyapa mamlaka makanisa mengine, kusamehe dhambi." Hayo ni katika ufafanuzi wa Kikatoliki.

112 Ukija kugundua, umwulize Mprotestanti, useme, "Mwamba huo ulikuwa nini?"

113 Wangesema, "Huyo alikuwa ni Yesu Kristo, ndiye mwamba." Loo, ndugu!

114 Yesu alisema nini juu yake? Petro alisema . . . "Mnasema ni nani?" Alisema, "Mnasema Mimi kuwa ni nani?" Hakuwa akiongea juu yake Mwenyewe. Alisema, "Mnasema Mimi kuwa ni nani?"

"Wengine walisema Wewe ni 'Musa,' na wengine wanasema Wewe ni 'Eliya.'"

"Lakini ninyi mnasema ni nani?"

Petro akasema, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

115 Akasema, "Heri wewe, Simoni Baryona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukuchukua theolojia ya mtu fulani kulihusu. Hukujifunza hili katika seminari. Lakini Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia hili. Na juu ya mwamba huu . . . " Haleluya! Mwamba gani? Ufunuo wa kiroho wa Mungu hujidhihirisha Mwenyewe kwa mtu binafsi. Haleluya! "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda."

116 Wakati mtu anapozaliwa kweli kwa Roho wa Mungu, na kuanzia utosi wa kichwa chake hata ncha za kucha za vidole vyake, amebadilishwa na Nguvu za ufufuo za Bwana Yesu Kristo. Nayo mawazo yake mwenyewe ya ubinafsi yamefifia, naye Mungu ana udhibiti kamili wa mtu huyo. Ataamini kila Neno lililoandikwa la Bwana Yesu Kristo, na kutenda vivyo hivyo.

117 "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Amina. Hilo lingekufanya ujisikie wa kidini, sivyo? Hakika lingekufanya!

> *Huyu ndiye jiwe* ambalo *lilidharauliwa na ninyi waashi,* . . .
>
> *Wala hakuna wokovu katika jina lingine lo lote,* isipokuwa Jina hili la Bwana Yesu; . . .

118 Nayo Biblia ilisema hapa, ya kwamba:

> . . . *waliona kuwa walikuwa* wasio na elimu wala maarifa . . .

119 "Walitoka shule gani? Kundi la punguani kutoka huko nje. Vema, kundi hili la watu wasio na elimu, wasio na elimu wala maarifa ni akina nani? Vema, hao watu hata hawajui ABC zao. Naam, angalia lugha wanayotumia, 'Tio, na aiko, na aiko, na tote na kuchota, na kuangamia.' Ni wa—watu wa aina gani hawa? Mbona, ulitoka katika seminari gani? Wewe ni Daktari nani?" Mnaona?

> . . . lakini iliwabidi *kuwafahamu*, kwa maana walitambua *kwamba walikuwa pamoja na Yesu.*

120 Hilo ndilo jambo kuu, ndugu. Kama huwezi kutofautisha kahawa na maharagwe yaliyopasuliwa; kama unamjua Bwana Yesu Kristo, na Nguvu za kufufuka Kwake, afadhali niwe na hizo kuliko kitu kingine chochote. Naam, bwana. Loo, jamani! Mungu, nitie nanga mle!

> Acha nipumzike chini ya Mti,
> Ambapo chemchemi hutiririka kwa njia huru,
> Ambapo Mwana-kondoo ndiye Nuru,
> Nayo nafsi ya aliyeokolewa haifi kamwe.

121 Hebu nitie nanga humo! Loo, jamani, jamani! Hebu niketi karibu na Mti usiokauka majani, wakati safari hii ya maisha itakapokwisha. Loo!

> Usitamani utajiri usio na maana wa ulimwengu huu,
> Ambao huoza upesi sana,
> Tafuta kupata hizo hazina za Mbinguni,
> Hazitapita kamwe!
>
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Shikilia mkono Wake usiobadilika! (Hiyo ni kweli.)
>
> Safari hii ikikamilika,
> Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
> Makao yako mazuri na yenye kung'aa ya Utukufuni,
> Nafsi yako iliyojaa furaha itayaona!

122 Moja ya siku hizi usiku, au moja ya asubuhi hizi, au moja ya adhuhuri hizi, nafsi yako itatengana na mwili wako, kama jino linalong'olewa. Unatembea kwenye nyuzi nyepesi ambazo zinaweza kukatika wakati wowote. Lakini ninajali nini? Unajali nini? Kwa maana Yeye atamwinua kwa mbawa Zake za milele. Atamshika, nafsi hiyo itakapotenganishwa kutoka hapa. Kutakuwa na Mtu atakayesimama mwishoni mwa barabara, jamani, jamani, kumchukua na kumkumbatia kwa mikono Yake ya milele, na kumpitisha katika bonde la uvuli wa mauti, kumleta huko, mkamilifu na asiye na lawama wala makosa, mbele za Baba. Basi kwa nini tuwe na wasiwasi? Kwa nini tuyajali yale ulimwengu unayosema, ama kile *hiki*, *kile*, ama

*kinginecho*? Maadamu tuna mkono wa Mungu usiobadilika ndani yetu wenyewe, tunajali nini?

123 Hebu watu, hebu kila mtu, hebu wanaume na wanawake, hebu watoto, hebu kila mtu hapa asiyemjua Bwana Yesu Kristo, anipe sababu kwa nini hupaswi kumtumikia. Nipe sababu kwa nini ungeweza kuachilia Krismasi hii ipite bila kumkubali Bwana Yesu Kristo. Acha kufikiria jambo *hili* au *lile*. Acha kufikiria kama "Nifanye *hivi* au nifanye *vile*?" Ninakuuliza jambo moja thabiti, je, umemwamini Bwana Yesu Kristo?

124 Kama kweli unaamini, nitathibitisha kwa Biblia kwamba una Uzima wa Milele wala huwezi kuangamia. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele." Yesu Kristo aliponena Maneno hayo! Petro alipoyanena, kwenye Siku ya Pentekoste! Yesu alipoyanena, papa hapa katika Yohana Mtakatifu 5! Walipoyanena, kote katika Biblia!

125 Mwanadamu ameyageuza, na kuyachanganyisha, na kujaribu kufanya *hivi* Nayo, na kufanya *hili*, kuyaunda madhehebu na kila kitu. Baadhi yao wamesema, "Naam, amini tu ya kwamba Yeye ni Bwana Yesu Kristo, kisha uingie. Hivyo tu." Mnaona hila za ibilisi? Mmoja alisema, "Loo, ndugu, tulifurahi sana, tukapaza sauti." Mnaona hila za shetani? Mmoja akasema, "Tulinena kwa lugha, nasi tunajua tumempokea." Mnaona hila za ibilisi? Mambo hayo ni sawa, lakini bado si Kristo. Hakika, ndivyo ulivyo.

126 Wakati mtu amemwamini Bwana Yesu Kristo kweli kweli, kabisa, ana Uzima wa milele, dakika anayoamini. Hiyo ni kweli, unapoamini! Maisha yako yataonyesha kile ulicho. Maisha yako!

127 Na hayo yote yatatukia. Mambo haya yote, kama kupaza sauti, na kushangilia, na kunena kwa lugha, na kuwaponya wagonjwa, na karama hizi zingine zote, na kadhalika, hazitakuwa kwa sababu ulifanya hivyo. Zitafuatana nawe, pamoja na ishara ya kweli ya Mungu. Unaona? Loo! "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake, mengine mtazidishiwa."

128 Ninapowazia juu ya ulimwengu huu unaoshindwa! Kisha ninaangalia pande zote na kuona maandiko ya mkono ukutani, juu ya kila taifa! Ninaona mabomu ya atomiki yamewafanya watu kutetemeka, wakati watawala wakuu na kadhalika . . . Mnapaswa kusoma wanachosema katika Pentagoni, kuhusu mambo haya kutimia. Mnapaswa kuona yale taifa hili . . . Ndugu, hebu nikwambie kitu, tunaweka ujasiri mkubwa sana mbele. Wakati, chini kabisa kwenye kiini cha taifa hili, wanaogopa sana. Mnajua hilo. Afadhali tukubali ukweli. Nanyi mna haki ya kuogopa sana.

129 Kuna mtu mmoja tu ambaye hana haki, hata kidogo, ya kuogopa, huyo ni mwanamume au mwanamke aliyezaliwa kwa

Roho wa Mungu. Bomu la atomiki ni tiketi ya kwenda mbinguni kwa mwaminio. Haleluya! Naam, bwana. Kifo hakiwezi kufanya lolote kwako ila . . . Kifo cha haraka ni Utukufu wa haraka. Hiyo ni kweli.

Joho hili la mwili nitaliangusha, na kufufuka
Na kunyakua tuzo ya milele,
Na kupaza sauti, wakati nikipitia hewani,
"Kwaheri, kwaheri, saa tamu ya maombi!"

130 Nimetoweka! Bomu la atomiki litamaanisha nini kwa watakatifu hawa wazee wenye mvi? Kijana mwanamume na mwanamke tena! Bomu la atomiki litamaanisha nini kwa makazi haya, na karibu wote wameondoka, nayo yameachwa upweke? Familia yote pamoja tena! Utukufu kwa Mungu, ndugu! Je, unaweza kuwa na nini zaidi ya hicho? Ukiwa na hakikisho kamili kwamba moyo wako unapumzika kule katika Kalvari, kwamba hakuna kitu duniani kinachoweza kukuchochea, kukubadilisha, kukutikisa!

131 Uko ndani ya Kristo Yesu, umetiwa nanga katika Ufalme wa Mungu, hata siku ya Ukombozi wako, uwasilishwe mbele Zake bila hatia. Si kile ulichofanya, "La—laiti ningeweza kuachana na *hili*, na laiti ningeweza tu kuachana na *lile*." Si chochote ambacho umefanya. Ni kile anachokufanyia. Je, unaamini kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa akili yako yote?

132 Wakati Petro alipokuwa anaenda, ama ninamaanisha . . . Filipo, alipokuwa akienda kumbatiza yule towashi. Alisema, "Haya hapa maji, ni nini kinanizuia nisibatizwe?" Petro . . .

133 Filipo akasema, "Ngoja kidogo. Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa akili yako yote! Kama unaamini!"

134 Akasema, "Ninaamini, kwa moyo wangu wote, nafsi yangu, na akili yangu yote, kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu."

Wakasimamisha gari; wakaingia majini, akambatiza.

135 Ndipo Roho Mtakatifu akamtwaa Filipo machoni pake, hata hakuona tena. Kisha akampeleka angani kwa yapata maili mia mbili, na kumketisha chini, na kuanzisha uamsho tena. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Mungu yule aliyeishi katika siku hiyo ni Mungu yeye yule leo.

136 Ninapomwazia Paulo huko nje kwenye ile meli usiku ule; matumaini yote yalikuwa yametoweka, wao kuwahi kuwa salama. Maskini meli hiyo ya kale ilikuwa imejaa maji, nayo ilikuwa katika hali mbaya sana. Matumaini yote, kila mtu, alikata tamaa. Naye Paulo akiwa ameketi kwenye nyumba ya sanaa usiku huo, labda akiomba.

137 Malaika wa Bwana akamjia, akasema, "Usiogope, Paulo. Usiogope, kwa maana nitakupeleka mbele ya Kaisari. Huna budi

kushuhudia huko. Na nimekupa kila mtu anayesafiri pamoja nawe.”

138 Ninaweza kumwona Paulo akikimbia mle melini, na kutikisa maskini mkono wake, na kupaza sauti, “Haleluya!” Akipiga makelele, “Ngojeni kidogo, ndugu zangu! Ngojeni kidogo!”

139 Wakasema, “Lo-loo, mtu fulani amechanganyikiwa sana hata amerukwa na akili.” Haya basi. Nao Madaktari wote wa Uungu wakatoka nje kuona imekuwaje.

Kasema, “Iweni na moyo hodari! Iweni na moyo hodari!”

140 Kasema, “Maskini jamaa huyu, ameingia kichaa huko. Hiyo hapo. Amekuwa akifunga kwa muda mrefu sana. Amefanya haya yote, na yuko karibu kuangamia sasa.”

141 Kasema, “Iweni na moyo hodari! Kwa maana jana usiku alisimama karibu nami Malaika wa Mungu, ambaye mimi ni mtumishi Wake, akisema, ‘Usiogope, Paulo, lakini lazima upelekwe mbele ya Kaisari. Na, hata hivyo, Mungu amekupa wale wote wanaosafiri pamoja nawe.’” Kasema, “Hata hivyo meli haina budi kuangamia kwenye kisiwa fulani, kwa maana niliiona katika ono. Lakini ninamwamini Mungu, ya kwamba itakuwa kama tu alivyonionyesha.” Nalo likatokea, neno kwa neno kwa neno, kikamilifu kabisa. Hiyo ni kweli.

142 Sasa, basi ninawatakeni muone kitu kidogo, ili mpate kuona upande wa pili, mandhari yake. Tazameni. Waliposhusha zile mashua na kuanza kuondoka kisiri, Paulo alisema, “Njia pekee ambayo mnaweza kuokolewa ni kubaki kwenye meli hii.” Ilibidi ufanye kulingana na BWANA ASEMA HIVI. Bwana alikuwa amewapa ono, lakini ilibidi ifanywe kulingana na njia Yake. Ndipo wakati . . .

143 Mungu hutoa kielelezo, cha kanisa la Roho Mtakatifu, ndugu, na jinsi ya kutoa kitu hiki kutoka kwenye machafuko. Unaweza kuwa na mabingwa wanne, na pentagoni, na kila kitu unachotaka kuwa nacho; unaweza kuweka wakfu makanisa na wahudumu, na kufanya theolojia na kuwaelimisha. Kamwe halitafanyika mpaka watu watakaporudi tena kwenye njia ya Milele ya Mungu, na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu; na kuendelea mbele, wakihubiri, pamoja na ishara na maajabu yakifuatana na huduma yao. Halitafanyika kwa chochote pungufu ya hiyo. Mungu anayo ratiba, lakini huna budi kuja kwenye hiyo ratiba.

144 Ee Mungu, tusaidie, usiku wa leo! Ndugu Neville! Tusaidie usiku wa leo kuamini hilo, ndilo ombi langu.

145 “Kwa maana hakuna wokovu katika jina lingine, ila katika Jina la Bwana Yesu.”

146 Sasa, tunapokaribia wakati wa Krismasi sasa, na hapa mambo yamepambwa kwa Baba Krismasi badala ya Yesu. Hata hawaandiki tahajia zake tena. “X-m-a-s.” Hata hawaandiki

"Kristo" tena katika Krismasi. Waliweka...Mbona, watu kamwe—kamwe hata hawafikirii juu ya kule kuzaliwa ama chochote kile, kwa Kristo, kwamba ni kwa sababu gani hasa. Jambo pekee wanalowazia, ni, Baba Krismasi alichukua mahali Pake. Na badala ya kushangilia chini ya Roho wa Mungu, wanatoka na kulewa na kushangilia. Mnaona? Hiyo ndiyo inayoleta tofauti.

147 Kwa hiyo, hata hivyo, ndugu, dada, siwezi kulikomesha hilo. Huwezi kulikomesha. Neno la Mungu lilisema itakuwa hivyo. "Watu watakuwa wenye kupenda anasa, kuliko kumpenda Mungu." Utalichambuaje hilo? "Wenye mfano wa utauwa." Kila mmoja wao huenda kanisani. Naam, bwana. "Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao ujiepushe nao."

148 Nina furaha sana usiku wa leo, rafiki Mkristo, kwamba niko hapa pamoja nanyi usiku wa leo. Nina furaha sana kwamba ni—nimekuwa na majaliwa ya kuzungumza nanyi, kwa moyo wangu.

149 Na moyo wangu wote umefungwa ndani ya Ujumbe huu. Umekuwapo tangu siku ile ile ambapo Mungu alinipa ubatizo wa Roho Mtakatifu, papa hapa Jeffersonville, Indiana, nilipomwamini Mwanawe, Yesu Kristo, na kumkubali hapa nje katika kibanda kidogo cha kale, kama Mwokozi wangu binafsi. Naye Bwana akanishukia usiku huo, na kutupa Nuru katika chumba hicho. Nami nikaitazama, huku nimeogopa sana hata nisingeweza kusogea. Nikapiga magoti kwenye gunia kuukuu la nyasi, kule chini kwenye Barabara Kuu ya Ohio. Nami nikaona hiyo Nuru ikifanya msalaba, na kitu Fulani kwenye msalaba huo kikinizungumzia. Tangu usiku huo, matumaini yangu hayajajengwa juu ya kitu chochote pungufu ya Neno la Mungu, na Yesu Kristo na haki. Hapo ndipo ninapoamini, kwa moyo wangu wote. Hima twendeni, hata iweje; tumaini langu bado liko pale pale.

150 Nami nina furaha, usiku wa leo, kuketi katika kundi kama hili, linaloamini jambo lile lile, lililompokea Bwana Yesu Kristo yeye yule.

> Kwa miaka mingi, kupitia hatari nyingi, taabu na mitego,
> Nimekuja tayari;

Imenifanya kuzeeka, imenivunja, imeniambua kabisa.

> Lakini ni neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,
> Neema ndiyo itakayonipeleka.

> Na wakati tumekuwa huko miaka elfu kumi,
> Tuking'aa sana kama jua;
> Hatutakuwa na siku chache zaidi za kuimba sifa za Mungu
> Kuliko saa tuliyoanza kwanza.

151 Danieli alipoona ono la hayo, ndipo akasema, “Ingawa wanatenda maovu, watafanya maovu katika siku za mwisho; lakini wale wamjuao Mungu wao watafanya mambo makuu katika siku za mwisho,” akizungumza juu ya wakati huu. Mnajua “mambo makuu” ni nini? Mambo makuu ya imani, watafanya ishara na maajabu. “Lakini waovu bado wataendelea kutenda maovu.” Kasema, “Watakimbia huku na huko, na maarifa yataongezeka. Lakini,” kasema, “kifunge Kitabu, ewe, Danieli. Utalala katika kura yako, lakini utasimama katika siku hiyo ya mwisho. Na wale walio na hekima watawavuta wengi kwa Kristo. Watang’aa kama nyota za mbinguni milele na milele.”

152 Miaka arobaini imenivunja vipande vipande. Miaka themanini labda imekuvunja vipande vipande. Labda miaka thelathini imefanya mtu tofauti kutoka kwako, muda kidogo tu wa wakati namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.]

153 Lakini je, uliwahi kuitazama nyota ya asubuhi inapochomoza asubuhi? Je, uliwahi kuamka mapema na kuitazama ikining’inia huko angani, wakati ikimetameta na kupaza sauti, na kushangilia angani? Haijawahi kupoteza hata chembe moja ya uzuri wake. Inang’aa na kupendeza tu kama ilivyokuwa siku ile Yeye alipoitundika, Mungu alipoitundika kwenye mzingo wake. Haijawahi kupoteza wakati wake wowote. Nayo imekuwa huko kupitia maelfu mara maelfu ya miaka, na kamwe haijapoteza uzuri wake.

154 Nayo Biblia inasema, “Wale wawaongozao wengi kutenda haki watang’aa kuliko nyota, milele na milele.” Haleluya! Ndugu, ni jambo jema kuwa mhubiri, hata hivyo, sivyo? Naam, ndivyo. Ni jambo jema kuwa Mkristo.

155 Nyakati zinaweza kuwa ngumu. Mungu hajaahidi maisha ya starehe, lakini ameahidi neema ya kutosha kwa kila jaribio linaloweza kukupata. Hiyo ni kweli. Naam, neema yatosha. Si kwamba ana starehe, maisha ya starehe, bali Yeye aliahidi neema ya kushinda katika kila jaribio. Wakati msalaba unapokuwa mzito, Kristo aliahidi kuwa pamoja nawe. Naam, bwana.

156 Siku moja tukufu, wakati yote yamekwisha, tutakutana Naye katika amani. Mungu ajalie kwamba kila mmoja wenu atapokea kitu kile kile.

157 Kukiweko na asiyeamini hapa, usiku wa leo, mwamini Bwana Yesu Kristo; na mara tu unapoamini, Mungu atakupa ushuhuda Wake. Atakutia muhuri katika Ufalme Wake milele. Ikiwa kuna kitu chochote kinachogonga moyoni mwako, na unakihisi, na unakataa kukipokea, utakuwa mwanamume na mwanamke mwenye mashaka hadi utakaposema, “Naam, Bwana Yesu.”

158 Nawe, kupitia juma hili lijalo, msimu huu wa Krismasi, wakati kila mtu ana furaha na kuimba, mmoja kwa mwingine; hebu wewe, kwa mikono. . .kama Simeoni wa kale, wakati msimu huo wa ajabu wa Krismasi, alipokuwa akipitia hekaluni, na kwa mikono yake yenye nguvu, loo, alimchukua Mwokozi mikononi mwake na kumkumbatia, kasema, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aende kwa amani, sawasawa na Neno Lako, kwa maana macho yangu yameuona wokovu Wako." Nawe, kwa mikono ya imani, vivyo hivyo, Krismasi hii, usikumbatie Baba Krismasi, au kubadilishana zawadi; lakini naomba umwalike na kumkumbatia moyoni mwako, kwa mikono ya imani, Bwana Yesu yeye yule ambaye Simeoni alimshika mikononi mwake miaka mingi iliyopita. Naye atakubariki na kukupa Uzima wa Milele. Wala huwezi kuangamia, kwa sababu una Uzima wa Mungu ndani yako.

159 Unajua kile neno. . .Sio kuingilia mambo ya Kiyunani. Hayo yatazungumziwa miongoni mwa watu wanaozungumza mambo ya Kiyunani. Hatuzungumzi mambo ya Kiyunani hapa. Tunazungumza Yesu Kristo, katika maskani hii. Hatuji na maneno makuu mno hapa. Tunakuja hapa bila kujua chochote ila Nguvu za kufufuka kwake Kristo. Lakini neno lenyewe, neno la Kiyunani, linamaanisha "Uzima wa Milele." Neno lile lile la Kiyunani, katika tafsiri. . .Ninazo za Kiebrania na Kiyunani, zote mbili, na nimezichunguza. Mimi si msomi katika hizo. Ninajua maneno machache tu, kitu cha kunisaidia. Mtu anapoanza kubishana, najua jinsi ya kuwakatisha kwa hilo. Lakini inapofikia mahali kama hapa, ambapo wakati. . .Neno lile lile la Kiyunani linalozungumza juu ya Uzima wa Mungu, huzungumza juu ya Uzima ule ule anaokupa. Na hayo yote mawili, maneno ya Kiyunani, na Uzima wa Mungu ama Uzima wa Milele, hutamkwa *Zoe*. Z-o-e, *Zoe*, "Uzima."

160 "Na wote wanijiao Mimi, nitawapa Zoe, Uzima Wangu Mwenyewe; nitawapa Uzima Wangu Mwenyewe, wala hawatapotea kamwe. Nami nitawafufua katika siku ya mwisho." Kwa maneno mengine, "Kila mtu ajaye Kwangu, nitamfunga ndani Yangu." Amina. "Naye atakuwa sehemu Yangu. Wala hawezi kufa zaidi ya vile ninavyoweza kufa, kwa maana Mimi sipatikani na mauti na siwezi kufa, nayo nafsi yake haipatikani na mauti wala haiwezi kufa. Nami nitamfufua tena siku ya mwisho." Hum! Loo, jamani!

161 Basi hiyo inatufanya tu, wakati maskini majaribu yanapokuwa magumu, kusema, "Ndani yangu mnakaa Roho wa Mungu. Hakuna jambo jema humu ndani ila Yeye aliye mle ndani. Mimi sio mali yangu mwenyewe; mimi ni Wake. Sitafuti mambo ya dunia. Ninamtazamia Yeye, kwa maana matumaini yangu yamejengwa juu Yake. Siku moja nitamwona, na hilo ndilo tu nililotamani. Ninaloishia, ni kuwaleta watu Kwake."

Nami nawaambia, maskini pingu hizo zinaanza kuanguka, nanyi mnaanza kutembea upya, tena.

162 Mungu awabariki. Natumaini kwamba mnaamini kwa moyo wenu wote. Wakati tukiomba:

163 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, usiku wa leo, kwa ajili ya Damu ya Mwanao mwenye haki, Bwana Yesu. Ninakushukuru Wewe, usiku wa leo, kwa ajili ya Roho Mtakatifu, na kwa kutembelewa Naye papa hapa katika jengo hili, na hata papa hapa sasa. Roho yule yule, kulingana na Neno la Mungu lisiloweza kukosea wala haliwezi kushindwa, Roho yule yule aliyemfufua Yesu kutoka kaburini, yuko papa hapa katikati yetu sasa.

164 Mungu, naomba watoto hapa ndani, wasiokujua Wewe, jalia walikubali, usiku wa leo, na kumwamini Bwana Yesu Kristo, na wawe na Uzima wa Milele. Lijalie. Jalia waamini wapate Uzima wa Milele, saa ii hii.

Waponye wagonjwa na wanaoteseka.

165 Kumbuka nyumba zilizofiwa, Bwana. Ee Mungu, na wakisimama karibu na majeneza, na labda wanaume na wanawake ambao hawajaokoka. Unaweza kusema nini? Huku ukijua ya kwamba Injili imehubiriwa moja kwa moja juu yao, mamia ya nyakati na mamia ya nyakati. Ee Baba, ninaomba ya kwamba wanaume na wanawake hapa watapata ono, usiku wa leo, na kutambua ya kwamba kila mmoja wetu ni mwanadamu, wala hatujui ni wakati gani tutakapoitwa kujibu huko ng'ambo hukumuni, na kutoa hesabu kwa yale tuliyofanya na Yesu Kristo. Halafu basi kesi inafungwa, kitabu kinafungwa; kinafungwa, wala hakuna kitu kinachoweza kufanywa. Tumejihukumu sisi wenyewe kwa kumhukumu Yeye.

166 Baba, loo, chunguza moyo wangu, usiku wa leo, Bwana. “Nichunguze,” alisema Daudi, “na unijaribu.” Si Daudi pekee, bali nasema jambo lile lile. Ikiwa kuna njia yoyote mbovu ndani yangu, Bwana, iondoe. Mungu, usiliache likawie karibu nami, Bwana. Silitaki. Silitaki, Baba. Liachilie.

167 Si kwa ajili yangu tu, bali kwa watu hawa wote walio hapa usiku wa leo, ambao wamenisikia nikihubiri, Baba. Ninaomba ya kwamba kama kukiwa na uovu wowote, dhambi yoyote, ndani ya watu hawa hapa, ya kwamba utawaondolea hayo yote, Bwana. Usiiruhusu ibaki karibu na hawa, watoto Wako. Mungu, iondolee mbali. Wape neema, washinde katika kila jaribio. Tujalie, Bwana. Jalia Uzao wa Mungu, kutoka katika Kikapu sasa, ukite mizizi katika mioyo ya watu, na kukua hata Uzima wa milele. Baraka hizi tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

> Loo, nataka kumwona, nataka kuutazama uso
> Wake,

Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye njia za Utukufuni nikainue sauti yangu;
Wakati masumbuko yote yamekwisha, na hatimaye niko nyumbani, nikafurahi daima.

Nisafiripo kwenye nchi hii, nikiimba safarini,
Kuwaelekeza watu Kalvari, kwa mtiririko Wako mwekundu,
Loo, mishale mingi huichoma nafsi yangu kutoka nje, ndani;
Lakini Bwana wangu huniongoza, sina budi kujishikiza Kwake.

Loo, nataka kumwona Yeye, niutazame uso Wake,
Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo.
Kwenye njia za Utukufuni nikainue sauti yangu;
Masumbuko yote yamepita, hatimaye niko nyumbani, kushangilia milele.

168 Loo, nataka kuimba, baadhi ya siku hizi. Ninaamini Bwana ataniruhusu niimbe, baadhi ya siku hizi. Naam. Nitakapovuka ule Mto, hiyo ni kweli, nitakapovuka ng'ambo ya pili. Labda sio upande huu. Siwezi kuimba. Lakini mnajua nitaimba wimbo gani?

Hakuna kitu kati ya roho yangu na Mwokozi,
Hakuna chochote cha ndoto danganyifu ya ulimwengu huu:
Nimeachana na anasa zote za dhambi,
Yesu ni wangu, hakuna kitu katikati. (Loo, jamani!)

. . . kati ya nafsi yangu na Mwokozi,
Hakuna chochote cha ndoto danyanyifu ya ulimwengu huu:
Nimeachana na anasa zote za dhambi,
Yesu ni wangu, hakuna kitu katikati.

169 Ni wangapi wanaoweza kuimba huo usiku wa leo, kama ushuhuda wakiwa wameinua mikono yao?

Hakuna kitu kati ya roho yangu na Mwokozi,
Hakuna chochote cha ndoto danganyifu ya ulimwengu huu:
Nimeachana na anasa zote za dhambi,
Yesu ni wangu, hakuna kitu katikati.

170 Je, hilo halikufanyi ujisikie kiajabu? "Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa

milele. Hataingia hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

171 Sisi hapa usiku wa leo, tumeinua mikono yetu, tuimbe, "Nimeachana na anasa zote za dhambi. Yesu ni wangu, hakuna kitu katikati. Kazi yangu, marafiki zangu, wapendwa wangu, watu wangu, mke wangu, watoto wangu, chochote kilichopo juu ya dunia hii, haijalishi ni nini, hakuna kitu kati ya nafsi yangu na Mwokozi. Yesu ni wangu, hakuna chochote katikati. Mambo mengine yote ni ya pili." Je, hiyo si ajabu sana?

172 Baadhi ya asubuhi hizi, ukisikia mtu akiimba "Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu," ukisha kuvuka Mto, unajua.

173 Mkifika Kule na kugeuzwa kuwa kijana mwanamume na mwanamke, mkikutana na vijana wenu wote Huko, mwajua. Na wapendwa wako, baba yako na mama yako, ukipeana mikono nao, ukisema, "Loo, mama, nafurahia kukuona tena. Vema, unaangalia kule, atakuja Ndugu John! Huyu hapa Ndugu Joe anakuja! Vema, angalieni hapa, si tuna wakati mzuri!"

174 Na huko nyuma kabisa juu ya kilima, huko mahali fulani, unasikia mtu fulani akiimba, "Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu, iliyomwokoa mwovu kama mimi." Unakimbia juu ya kilima na kuangalia, unaona kile kibanda kidogo kule pembeni, Ndugu Branham atakuwa amesimama pale nje akiimba, "Neema ya Ajabu."

175 Unasema, "Naam, utukufu kwa Mungu! Alifika Nyumbani. Huyo hapo, akiimba, *Neema ya Ajabu*." Loo, jamani!

> Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, lakini sasa mimi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

176 Ilikuwa ni kwa neema! Kule nyuma kabisa kabla ya ulimwengu kuumbwa, Mungu akizungumza na viumbe Vyake vya Kimalaika, kasema, "Nitakuwa na mtu anayeitwa William Branham akihubiri Injili."

> Neema ndiyo iliyoufundisha moyo wangu kuhofu,
> Neema ndiyo iliyoondoa hofu zangu;
> Jinsi hiyo neema ilivyoonekana ni ya thamani
> Ile saa . . . (Sasa nini?) . . . nilipoamini kwanza!

> Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
> Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
> Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,
> Kwani alinipenda kwanza.

> Sitamwacha kamwe,
> Sitamwacha kamwe,

Sitamwacha kamwe,
Kwani alinipenda kwanza.

Nina Baba huko ng'ambo,
Nina Baba huko ng'ambo,
Nina Baba huko ng'ambo,
Kwenye Ufuo wa pili.

Loo, siku moja angavu nitaenda na kukutana Naye,
Siku moja angavu nitaenda na kukutana Naye,
Siku moja angavu nitaenda kukutana Naye,
Kwenye Ufuo wa pili.

Loo, huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Huo si utakuwa ni mkutano wenye furaha!
Juu ya Ufuo wa pili.

Kweli, siku hiyo angavu inaweza kuwa kesho,
Siku hiyo angavu inaweza kuwa kesho,
Siku hiyo angavu inaweza kuwa kesho,
Kwenye Ufuo wa pili.

177 Hiyo si itakuwa ya ajabu? Nampenda "Baba."

Baba yangu ni tajiri wa nyumba na mashamba,
Yeye anashikilia mali ya ulimwengu mkononi Mwake!
Wa yakuti na almasi, ya fedha na dhahabu
Hifadhi Zake zimejaa, ana mali isiyoweza kuelezeka.

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

Hema au nyumba ndogo, kwa nini nijali?
Wananijengea jumba la mfalme Kule!
Ingawa nimefukuzwa nyumbani, lakini bado ninaweza kuimba:
Loo, utukufu kwa Mungu, mimi ni mtoto wa Mfalme!

Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Mimi ni mtoto wa Mfalme!
Pamoja na Yesu Mwokozi wangu,
Mimi ni mtoto wa Mfalme!

178 Baba yetu wa Mbinguni, mioyo yetu inaposukumwa na nyimbo hizi za zamani ambazo ziliandikwa na Roho Mtakatifu, miaka mingi, mingi iliyopita, wakati ndugu ambao wameondoka, walikuwa wamepata ono. Tunazipenda, kwa kuwa zinatupa msingi thabiti katika nyakati hizi za taabu. Mungu, jalia, usiku wa leo, kwamba dhambi zote zitaondolewa

kwetu sasa. Tunapoingia wakati wa Krismasi, ondoa dhambi, ondoa magonjwa, Bwana. Mungu, wabariki wahitaji usiku wa leo, kila mahali. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu.

179 Kuna watu sasa ambao wangependa kupenya hadi madhabahuni, kutiwa mafuta na kuombewa. Mnaweza kuja tunapouimba wimbo huu, *Mtoto Wa Mfalme*, tena. Mnaona? Ikiwa umesimama upande huu. . .

54-1219E Matendo Ya Roho Mtakatifu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org